# NINAANZAJE SEKONDARI KWA MAFANIKIO.

*"Kitabu Elekezi kwa Wanafunzi Wanaotarajia Kuanza Elimu ya Sekondari;"*

**Brother Elihuruma Maruma**

**TOLEO LA KWANZA**
Oktoba 2021

Kitabu hiki kimeandikwa na
Bro. Elihuruma Maruma

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhisiwi kunakili, kurudufisha au kutumia kitabu, au sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mmiliki. Kufanya hivyo ni kuvunja sharia na haki ya mwandishi na mchapishaji; na ukiukwaji wa taratibu hii unaweza pelekea mashitaka toka kwa waandaaji wa kazi hii.

ISBN 978-9987-7894-0-5

Kitabu hiki (pamoja na jalada) kimesanifiwa,
kupangiliwa na kupigwa chapa na
Pathfinderimage - Morogoro
Simu: 0693 274 740

Mawasiliano
Bro Elihuruma Maruma
Simu: +255 752 307008

*Kwa ajili yako*

______________________________

*kutoka kwa*

______________________________

# TABARUKU

Kwa Mdogo Wangu Unayesoma Kitabu Hiki, Naomba Nikuhakikishie Tu Kwamba Ukizingatia Yaliyomo USHINDI Na KUFANIKIWA Ni Lazima. Mimi Nilishinda, Na Wewe Utashinda Tena Zaidi Yangu.

# SHUKRANI

1. Kwa Mungu Aliyenipa Neema Hii Ya Kuona Umuhimu Wa Kuyagusa Maisha Ya Wahitimu Wa Darasa La Saba Ili Wazifikie Ndoto Zao Kwa Kuanza Sekondari Kwa Ushindi.
2. Familia Yangu Ambayo Imekubali Kunipa Muda Wa Kuyagusa Maisha Ya Wengine, Kwa Kujua Na Kwa Kutokujua.
3. Caroline Richard Na Joshua Richard Kwa Kukubali Picha Zao Kutumika Katika Kava La Kitabu Hiki, Zaidi Wazazi Wao Walioniruhusu Kutumia Picha Za Vijana Wao Hawa.
4. Ambwene Nkwera Kwa Kuchapa Na Kupitia Kitabu Hiki, Pamoja Na Esuvath Richard Kwa Kukubali Kusimamia Zoezi La Kuwezesha Maandalizi Ya Kitabu Hiki.
5. Kila Mmoja Anayehusika Katika Mauzo Na Manunuzi Ya Kitabu Hiki Ukiwemo Wewe Unayesoma Sasa Kitabu.

Ahsanteni Sana!.

# Yaliyomo

*Tabaruku*........................................iv
*Shukrani*..........................................v

Kujenga Msingi na Kanuni ya Pembetatu.1

Elimu ya Sekondari na Masomo yake ....12

Dira, Ndoto na Malengo yako................22
Mambo 7 ya Msingi ya Kuzingatia
Shuleni ................................................30

Makosa Makubwa 18 yanayosababisha
wengi Kufeli ..........................................52

Misisitizo Thabiti-Nguzo Kubwa 10
za Kukufanikisha ...................................61

Maswali Muhimu ya Kujiuliza
Unapoelekea Sekondari. .........................66

**SURA YA 1**

# KUJENGA MSINGI na KANUNI YA PEMBETATU.

***"Tena ujapokuwa huo mwanzo wako ulikuwa mdogo, Lakini mwisho wako ungeongezeka sana" Ayubu 8:7.***

Wakati ulipokuwa mdogo sana ilikuwa ni ngumu sana kwako kujua kwamba ipo siku utahitimu Elimu ya Msingi na kisha utaanza Elimu ya Sekondari. Chukulia ulipokuwa **CHEKECHEA**, Je wakati huo ulishawahi kuwaza kwamba utakuja kusoma Elimu ya Sekondari? La hasha, Ila leo tayari wewe ni mwanafunzi aidha mtarajiwa au tayari upo shule fulani ya Sekondari.

BIBLIA imesema vizuri hapo juu kwamba **MWANZO** ulikuwa **MDOGO** lakini **MWISHO** utakuwa **MKUBWA**. Ulianza darasa la kwanza ulikuwa mdogo sana lakini leo tayari unaitwa mwanafunzi wa Sekondari. Ni vizuri nikupongeze kwa kuhitimu vizuri Elimu ya Msingi lakini pia nikupongeze na kukukaribisha kwenye Elimu ya Sekondari. Elimu itakayokupeleka kwenye hatma

nzuri na ya mafanikio kwennye maisha yako yote.

Jambo la Kwanza la Msingi **FAHAMU KWAMBA** haukumaliza Elimu ya msingi kwa Nguvu zako au kwa sababu ya akili nzuri uliyonayo bali ni **UPENDO** na **MPANGO MZURI** wa **MUNGU** maishani mwako, amekuwezesha haya yote. Hebu tumia muda huu kabla hujaendelea kusoma kitabu hiki Elekezi Kumshukuru Mungu.

Jambo la Pili, **ELEWA NI MPANGO WA MUNGU WEWE KUSOMA SEKONDARI**, Hii ni hakika na kweli. Maadam Mungu amekupa uhai na afya njema, na amekuwezesha kufaulu basi tambua ni wazi kwamba **ANATAKA USOME SEKONDARI** na si kusoma sekondari tu bali **ANATAKA** pia **UFAULU** na **USONGE MBELE ZAIDI** na **ZAIDI.**

Jambo la Tatu**, NI LAZIMA UJENGEWE MISINGI IMARA** na **UPEWE MAELEKEZO SAHIHI** tena na watu sahihi yatakayokusaidia kuanza Elimu ya Sekondari na Kufaulu vizuri. Siku hizi kumekuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaofeli vibaya Sekondari na hii ni kwa sababu hawakujengewa misingi sahihi na Imara **LAKINI** pia hawakupewa maelekezo sahihi ya kuwasaidia

kufaulu kwenye masomo yao ya Sekondari.

## FAIDA YA KUJENGA MSINGI IMARA

Nyumba yoyote hata kama ingekuwa na uzuri wa kiasi gani katika muonekana wa nje, kama itakuwa haikujengwa katika misingi imara ni lazima tu siku moja itabomoka, kuharibika na mahali pake hapataonekana tena. Hali kadhalika na Wewe vile vile kama mwanafunzi wa sekondari ikiwa hautajengewa misingi imara hapa mwanzoni, ni dhairi hautafanikiwa na hii haijalishi ulikuwa unaongoza kiasi gani darasani ulipokuwa shule ya msingi, ama ulifaulu kwa wastani mkubwa kiasi gani kwenye mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba.

Wakati tunasoma Sekondari tulikutana na wanafunzi wengi waliokuwa wamefaulu vizuri shule ya msingi na hasa ule mtihani wa mwisho wa Taifa, Na wengine walikuwa wakiongoza vizuri kwenye shule za Msingi wanazotoka lakini mwisho wa siku waliambulia kufeli vibaya sekondari.

**KUMTEGEMEA na KUMTII MUNGU** ni **KUJENGA MSINGI MKUBWA NA IMARA.**

***"Wamtumainio Bwana ni kama mlima Sayuni, Ambao hautatikisika, wakaa milele" Zaburi 125:1.***
Moja ya mambo makubwa na ya msingi tena ya kuyafahamu mapema ni suala la Kujenga msingi wa **KUMTEGEMEA MUNGU** kwenye masomo yako na kwenye mambo yako yote. Unapoamua kuchagua na kumaanisha kumtegemea Mungu, Biblia inasema hautatikisika bali utakaa milele, Hebu angalia tena:

***"Mtumaini BWANA kwa Moyo wako wote wala usizitegemee akili zako mwenyewe, katika njia zako zote mkiri yeye, naye atayanyoosha mapito mapito yako" Mithali 3:5-6.***

Tuliwaona wengi ambao walikuwa na akili sana za Darasani, Na hawakumtegemea wala kumtumaini Mungu na mwisho wa siku walifeli vibaya na kupoteza Dira au Mwelekeo wa Masomo yao. Na ndio maana ni lazima sasa uchague na umaanishe kutoka moyoni mwako kumtegemea na kumtumaini Mungu.  Na Mungu anaweka wazi kwa wale wasiomtegemea anasema

"………..***Maana pasipo mimi ninyi hamuwezi kufanya jambo lolote" Yohana 15:5***

***"Bwana asipoijenga nyumba, wajengao wafanya kazi bure, Bwana asipoulinda mji waulindao wakesha bure" Zaburi 127:1***

Na kwa wanaomtegemea anasema vizuri sana, Eti anakwambia hivi.

***Yeremia 17:7-8 "Lakini amebarikiwa Yule mtu ambaye tumaini lake ni katika BWANA ambaye matumaini yake ni katika BWANA. Atakuwa kama mti uliopandwa kando ya maji uenezao mizizi yake karibu na kijito cha maji. Hauogopi wakati wa joto ujapo, Majani yake ni mabichi daima. Hauna hofu katika mwaka wa ukame na hautaacha kuzaa matunda."***

Tafsiri yake ni nzuri sana mdogo wangu, yaani anasema **UTAFANIKIWA** ukimtegemea Mungu na unafananishwa na mti uliopandwa karibu na chemchem za maji, haijalishi hali itakuwaje ya kimasomo kwa wengine, lakini kwako kwa hali yoyote anasema **KUFANIKIWA NI LAZIMA** (**Hautaacha kuzaa matunda**)

# MUNGU ANAZO MBINU ZA KUKUFANIKISHA

Ni faida sana KUMTEGEMEA MUNGU maana yeye ni Mungu mkuu mwenye Nguvu, Uwezo, Mamlaka na Ahadi za kweli za kukusaidia kufaulu kwenye masomo yako, na hata kwenye jambo lolote maishani mwako. Sio wazazi wako, waalimu wako, marafiki zako au mtu yeyote yule anayeweza kukufanikisha isipokuwa Mungu peke yake. Na ndio maana Biblia inaweka wazi jambo hili ikisema,

***"Najua kuwa hakuna lisilowezekana kwa Mungu" Luka 1:37***

***"Najua ya kuwa waweza kufanya mambo yote………" Ayubu 42:2***

***"Maana yeye alisema, ikawa; Na Yeye aliamuru, ikasimama." Zaburi 33:9.***

***"Tazama, mimi ni BWANA Mungu wa wote wenye Mwili; Je! Kuna gumu lo lote nisilo liweza?" Yeremia 32:27***.

Hizi si hadithi au mambo ya kudhania tu, Ni kweli na dhairi kabisa kwamba **HAKUNA CHA KUMSHINDA MUNGU,** Na hii haijalishi vile

ulivyo au namna unafikiri bali unahitaji kukubali na kuwa tayari kumtegemea ili uone namna atakavyokutendea kwenye masomo yako na maisha yako kwa ujumla.

## ANATAKA TU UMTII NA KUMPENDA

Ili umuone Mungu akikusaidia na kukuwezesha kwenye masomo yako ya Sekondari ni lazima **UMTII** na **UMPENDE** kwa moyo wako wote. Na unajua wazi kwamba hakuna mtu anaweza kukusaidia kama haumtii, haumheshimu na wala haumpendi, Na tena haumsikilizi na mbaya zaidi hauna muda nae. Fahamu na Elewa hili kwa kina kwamba MUNGU anao mpango mzuri na maisha yako na ndio maana anasema hivi kwenye;

*Yeremia 29:11-13*“***Maana nayajua mawazo ninayowawazia ninyi, asema Bwana, ni mawazo ya amani wala si mabaya, kuwapa ninyi tumaini siku zenu za mwisho. Nanyi mtaniita, mtakwenda na kuniomba, nami nitawasikiliza. Nanyi mtanitafuta na kuniona, mtakapo nitafuta kwa moyo wenu wote”.***

Ili uone msaada na ukuu wa Mungu kwenye masomo yako ni lazima UMTII kwa kuzishika na kuishi sawasawa na amri zake. Kwa kufanya hivyo anasema ukimuita na kuhitaji msaada wake atakusikia na kufanya. Hebu **sema "SIRI NI UTII KWA MUNGU"** na "**UFUNGUO WA KUFANIKIWA NI KUMPENDA MUNGU".**

***"Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito"***
***1 Yohana 5:3.***

Kumpenda Mungu ni kule kuzishika amri zake kwa kumaanisha, **Lakini Zaidi** Kumpenda Mungu ni kule kupata muda mara kwa mara na Mungu kwa kulisoma na kulitafakari **NENO LAKE (Biblia)** pamoja na kuongea nae kwa njia ya **MAOMBI.** Ukimpenda Mungu atakupatia mema na ukimtwika kila jambo atakufanya kichwa na wala si mkia.

***"Nasi twajua katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema yaani wale walioitwa kwa kusudi lake"***
***Warumi 8:28***

***"Bwana atakufanya kuwa kichwa, wala si mkia; nawe utakuwa juu tu wala huwi chini;***

*utakapoyasikiliza maagizo ya BWANA, Mungu wako, nikuagizayo hivi leo, kuyaangalia na kuyafanya" Kumb 28:13*

## KANUNI YA PEMBETATU

Hii ni kanuni ya ajabu na inayoumiza, lakini itakusaidia sana kujua ni kwa nini moja ya mambo unayohitaji sana kwenye Elimu yako ya Sekondari ni **MUNGU**. Ni ukweli usiopingika kwamba **ELIMU YA TANZANIA** imekaa kama pembetatu, Kwa nini imekaa kama pembe tatu? Ni kwa sababu idadi ya wanaosoma huzidi kupungua kwa kadri ya viwango vya Elimu vinavyo ongezeka. Kwa mfano tu, Idadi ya wanafunzi wanaosoma Elimu ya Msingi ni kubwa kuliko Wanafunzi wanaosoma Elimu ya Sekondari mpaka kidato cha Nne, Na Idadi ya wanafunzi wanaosoma Elimu ya Sekondari hadi kidato cha Nne ni kubwa kuliko wanaosoma kidato cha Tano na Sita. Halikadhalika Idadi ya Wanaosoma chuo kikuu ni ndogo sana ukilinganisha na wanaomaliza kidato cha sita.

# HII INA MAANA GANI?

Hii inamaanisha kwamba kuna idadi kubwa ya wanafunzi wanaofeli kutoka kiwango kimoja cha Elimu hadi kingine cha juu zaidi. Na ili uwe mmoja ya wale wanaoendelea kwenda juu na sio wale wanaobaki (Wanaofeli) **Unahitaji Kumtii, Kumpenda** na **Kumtegemea Sana Mungu.**
Hebu Angalia hii pembetatu hapa chini




Kisha jitazame wewe ukiwa na kiwango cha juu kabisa cha Elimu, Kwenye ile ncha ya juu ya Pembetatu kwa sababu tu ulichagua kujenga msingi wako tangu unaanza Sekondari kwa Kumtegemea, Kumpenda na Kumtii Mungu. Kwa akili zako tu hutaweza kufika hapo juu ILA Ukimtegemea Mungu **YOTE YANAWEZEKANA.**

Ikiwa umeamua sasa kuanza Elimu ya Sekondari kwa kujenga msingi wako kwa kumtegemea Mungu hebu sema ukiwa unasoma haya maelezo hapa chini:

***Mimi……………………………………… nimeamua KUKUKIMBILIA na KUKUTEGEMEA Mungu wangu Yehova Katika Yesu Kristo ili nisiaibike wala nisifeli popote. Ninatubu dhambi zangu na makosa yangu yote kwa Damu ya Yesu, Ninaomba unisamehe Ee BWANA. Karibu Roho Mtakatifu ndani yangu nifundishe kumpenda na kumtii Mungu tangu sasa na hata milele. Ninaanza masomo yangu ya Sekondari katika uweza na nguvu za MUNGU, Amina.***

SURA YA 2

# ELIMU YA SEKONDARI NA MASOMO YAKE

*"Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa Kiasi" 2 Timotheo 1:7*

***"usiogope maana mimi ni pamoja nawe; usifadhaike, kwa maana mimi ni Mungu wako; nitakutia nguvu, naam, nitakusaidia, naam, nitakushika kwa mkono wa kuume wa haki yangu" Isaya 41:10***

Ipo tofauti kubwa kidogo kati ya masomo ambayo yanafundishwa Sekondari na ambayo ulikuwa ukifundishwa ulipokuwa Elimu ya Msingi. Utofauti huu haumaanishi ni **UGUMU**. Tutakueleza vizuri tena kwa kina juu ya masomo ambayo unakutana nayo Sekondari. Kwa kweli ni masomo mazuri na marahisi sana na tena mengine yanafanana na yale ambayo uliyoyapitia shule ya msingi.

Kwenye sura ya kwanza tulikufundisha umuhimu wa wewe kumtegemea Mungu. Na hayo maandiko hapo juu yanaweka dhahiri kwamba Mungu hakutupa

roho ya woga na ndio maana anasisitiza akisema **USIOGOPE** kwa maana nyingine anataka UWE JASIRI unapoanza Elimu ya Sekondari maana Yeye yu pamoja nawe. Hivyo basi wewe ni mlima Sayuni hautatikisika kamwe, eti kwa sababu ya hii tofauti iliyopo kati ya masomo ya shule za Msingi na haya ya Sekondari. Hebu sema "**SIOGOPI MASOMO YA SEKONDARI, MAANA MUNGU YU PAMOJA NAMI**".

## MASOMO YA SHULE YA MSINGI

Kwa wale mliosoma masomo ya shule za msingi za kawaida ambazo sio zile za "English Medium" mlikuwa mkisoma masomo karibia yote kwa **KISWAHILI** isipokuwa somo moja la Kiingereza. Na masomo mliyokuwa mkijifunza ni Hisabati, Sayansi, English, Stadi za Kazi, Maarifa ya jamii na mengine kutegemea na shule uliyosoma. Mambo mengi mliyokuwa mkifundishwa humu utajifunza tena sekondari, isipokuwa kitakachobadilika zaidi ni Lugha tu toka Kiswahili kwenda Kingereza.

Na ashukuriwe Mungu kwamba hata Mimi niliyekuandikia kitabu hiki nilisoma shule za Msingi za kawaida kabisa na tulipoenda Sekondari pamoja na badiliko hili la lugha ya Kiingereza bado tulikuwa

tukifaulu sana na wakati mwingine kuliko hata wale waliosoma "English Medium" **KAA MKAO WA KUFAULU**. Hebu sema tena **"SIOGOPI MASOMO YA SEKONDARI**."

## MASOMO YA SEKONDARI

Unapoanza Elimu ya Sekondari ni lazima ufahamu masomo utakayosoma, tena ni muhimu upate picha kamili ili mtu awaye yeyote asikudanganye chochote na kukukatisha tamaa.

**MASOMO YA SEKONDARI** yamegawanyika kwenye makundi mbalimbali kama ifuatavyo: -

1. **MASOMO YA SAYANSI** [Science Subjects]
2. **MASOMO YA SANAA** [Arts Subjects]
3. **MASOMO YA BIASHARA [**Commercial Subjects]
4. **MASOMO YA KILIMO [**Agricultural Subjects]
5. **MASOMO YA UFUNDI [**Technical Subjects]

# 1. MASOMO YA SAYANSI [SCIENCE SUBJECTS]

Kuna masomo mbalimbali ya sayansi unapoingia sekondari masomo hayo ni kama yafuatayo:

## (i)PHYSICS [Fizikia]

***Physics is the study of matter in relation to energy.*** Fizikia ni somo la Sayansi inayohusiana na mambo ya maada ikihusiana na nishati mbalimbali. Ndani ya somo hili utajifunza mambo mengi mazuri ya maada na nishati na huku ukipata nafasi ya kuelewa zaidi kwa habari ya vipimo na hesabu mbalimbali. Ni somo zuri sana, rahisi ila tu linahitaji umakini mkubwa unapofundishwa.

## (ii)CHEMISTRY [Kemia]

***Chemistry is the Study of composition and decomposition of matter***. Kemia ni somo la sayansi inayohusiana na utengenezaji na kuharibiwa kwa maada. Humu utajifunza mambo mengi mazuri yanayohusiana na Hali za maada, Aina za maada na zaidi namna mbalimbali ambazo maada hutengenezwa na hata kuharibiwa. Ni somo rahisi, zuri na la kuvutia mno.

## (iii)BASIC MATHEMATIC [Hisabati]

***Mathematics is the Study of numbers and calculations.*** Hisabati ni somo la namba na kukokotoa. Ni moja ya masomo ambayo wanafunzi wengi huzembea na kuliogopa mapema na hii huwafanya wengi kufeli sana. Ila sasa kwako UKWELI NI HUU, Hisabati ni somo zuri jepesi na la kuchangamsha. Unachotakiwa kufanya ni kumsikiliza mwalimu kwa umakini na kufanya mazoezi ya kutosha na ZAIDI kutokata TAMAA kivyovyote vile.

## (iv)BIOLOGY [Baolojia]

***Biology is the Study of living things or living organism and non-living things.*** Baiolojia ni somo la Sayansi inayohusiana na viumbe hai. Ni somo ambalo ndani yake utajifunza mengi yanayohusiana na viumbe hai kama sifa zao, tabia zao, makundi yao na hata mifumo yao. Ni moja kati ya masomo rahisi sana na yanayopendwa mno.

# 2. MASOMO YA SANAA [ARTS SUBJECTS]

Masomo ya Sanaa utakayoyasoma Sekondari ni haya hapa:

## (i)HISTORY [Historia]

***History is the Study of past, present and future human activities.*** Historia ni somo la sanaa linalohusiana na shughuli mbalimbali walizofanya wanadamu waliopita, waliopo na watakaokuja. Ni somo la kuvutia litakalokusaidia kujua juu ya mambo mbalimbali ya miaka mingi iliyopita, jinsi wanadamu walivyoishi, wanavyoishi sasa na hata baadae. Historia ni moja pia ya masomo ya kuvutia, kushangaza na kufaulu kwa urahisi.

## (ii)GEOGRAPHY [Jiografia]

***Geography is the Study of man and his environment.*** Jiografia ni somo ambalo huingia kwenye makundi mbalimbali kwa sababu uhusiana na binadamu, mazingira yake na shughuli zake pia. Na hii ndio maana huchukuliwa pia kama somo la sayansi, sanaa na hata uchumi. Humu utajifunza mengi kuhusu mazingira yanayotuzunguka kwa ujumla kama Bahari, Maziwa, Mito, Milima lakini pia utajifunza

juu ya shughuli mbalimbali wanazofanya wanadamu na mengine mengi. Ni somo rahisi, zuri na la kuvutia pia.

## (iii) CIVICS [Uraia]

***Civics is the Study of human rights and responsibilities of citizen.*** Uraia ni somo la sanaa linalohusiana na haki na wajibu wa raia. Kwenye hili somo utajifunza mambo mengi yanayohusiana na Taifa letu lakini pia utaelewa haki na wajibu wako kama raia wa Tanzania huku ukielewa kuhusu katiba na mambo yanayofanana na hayo. Ni somo zuri, rahisi na litakalokusaidia sana kujitambua wewe kama raia wa Tanzania.

## (iv)ENGLISH [Kiingereza]

***English is subject is about syntax, grammer, literature on English language.*** Kingereza ni somo la lugha ya kingereza ambalo utajifunza juu ya sarufi, uandishi, matamshi na mambo yote muhimu yanayohusiana na lugha ya kiingereza. Kumbuka karibu masomo yote ya sekondari hufundishwa kwa lugha hii hivyo ni muhimu sana kuzingatia kujifunza kuongea na kuandika lugha hii kwa bidii. Kingereza pia ni somo zuri na rahisi kujifunza.

## (v)KISWAHILI

Kiswahili ni somo linalohusiana na sarufi, uandishi na mambo mengine mengi juu ya lugha yetu ya Kiswahili. Hili ndilo somo pekee linalofundishwa kwa lugha ya Kiswahili, ni somo zuri na rahisi ila linahitaji umakini mkubwa wa kufuatilia kipengele kwa kipengele ili kufaulu kwa kiwango kikubwa sana.

# 3. MASOMO YA BIASHARA [COMMERCIAL SUBJECTS]

Masomo haya ya Biashara si lazima ukutane nayo kila shule ILA kuna baadhi ya shule ambazo hufundisha masomo haya. Masomo haya huwa ni mawili ambayo ni:

## (i)BOOKEEPING

***Book keeping is the art of recording financial business transaction in the set of books in terms of money or money's worth.*** Hili linausiana moja kwa moja na kanuni na taratibu za kutunza kumbukumbu za kifedha na rasilimali zingine.

## (ii)COMMERCE

***Commerce is the study of exchange and distribution of goods and services from the point of production to the point of consumption to satisfy human wants.*** Hili linahusiana na mfumo, taratibu na kanuni mbalimbali za biashara ikiwemo mifumo, aina na njia mbalimbali za Kibiashara kuanzia usambazaji wa bidhaa na huduma kutoka kwa mzalishaji mpaka kwa mlaji.

# 4.MASOMO YA KILIMO [AGRICULTURAL SUBJECTS]

Somo la Kilimo huwa ni moja tu na kwa kawaida si kila shule utakayoenda litakuwa linafundishwa, ila tu kuna baadhi ya shule chache sana kwa sasa ambazo hufundisha hili somo. Somo hili linaitwa;

## (i)AGRICULTURAL SCIENCE [Sayansi ya Kilimo]

***Agriculture is the science, art and practice of cultivating plants and livestock.*** Ni somo linalohusiana na mambo yote yanayohusiana na Kilimo na mifugo. Mbinu, kanuni na taratibu mbalimbali za kuwezesha uzalishaji mkubwa wa Kilimo na Ufugaji. Ni somo zuri sana.

# 5.MASOMO YA UFUNDI [TECHNICAL SUBJECTS]

Haya ni masomo ambayo utakutana nayo ikiwa utaenda shule za ufundi. Na kwa hiyo basi kwa sasa yafahamu tu kwamba kuna masomo ya ufundi wa aina mbalimbali. Haya ni masomo yanayohusiana na ufundi wa mabomba [Plumbing], Umeme [Electrical], Useremala [Capentry] na aina nyingine nyingi za ufundi.

## MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIA

1. Masomo yote hufundishwa kwa lugha ya Kiengereza isipokuwa somo la Kiswahili.
2. Masomo yote ni Muhimu sana kwako, Hivyo ni muhimu sana uyape yote Kipaumbele katika kusoma.
3. Jijengee Mtazamo wa Kuyapenda mosomo yote na WALIMU wako wote.

SURA YA 3

# DIRA, NDOTO na MALENGO YAKO

Ni muhimu sana tusaidiane pia juu ya uhusiano uliopo juu ya Dira, Ndoto na Malengo uliyonayo juu ya maisha yako **NA** masomo unayosoma Sekondari. Ni muhimu sana kila mwanafunzi ajue dira [Mwelekeo wa Maisha] ndoto [Kile unachopenda kufanya baadaye] ili hii ikusaidie kuweka msisitizo juu ya masomo fulani fulani wakati unapokuwa Sekondari.

Duniani kuna wataalamu na watu wanaofanya kazi mbalimbali. Kwa mfano kuna:

1. Madaktari wa Binadamu.
2. Madaktari wa Wanyama.
3. Wafamasia (Wataalam wa madawa).
4. Wanasheria (Mawakili, Mahakimu, Majaji).
5. Walimu.
6. Marubani
7. Wahasibu
8. Wanauchumi
9. Maaskari
10. Wanajeshi

11. Wahandisi Mbalimbali
12. Wanasaikolojia
13. Wanasiasa
14. Wachungaji [Watumishi mbalimbali wa Mungu]
15. Mafundi mbalimbali
16. WafanyaBiashara
17. Manesi (Wauguzi)
18. Wataalamu wa Maaabara
19. Wabunifu wa Majengo

Hizi ni baadhi tu ya kazi za namna mbalimbali kulingana na utaalamu wa namna mbalimbali, watu wanazofanya. Na unachotakiwa kujua ni kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya masomo unayosoma na utaalam [Kazi] mbalimbali kama nitakavyokueleza hapo mbele.

## NDOTO YAKO NA MASOMO YAKO

***"Nitakufundisha na kukuonyesha njia utakayoiendea, nitakushauri jicho langu likikutazama" Zaburi 32:8***

Kwa kuwa ulimchagua na kuamua kumtegemea na kumtii Mungu, Yeye anasema yupo tayari kukufundisha na kukuonyesha njia utakayotakiwa kuendelea, na yupo tayari kukushauri na kuona kwa

karibu kile unachofanya unapokuwa Sekondari.

Ukumbuke tu kwamba ni muhimu sana kusoma masomo yote kwa bidii ili kupandisha kiwango chako cha ufaulu, Lakini pia ni hekima kufahamu masomo yote yatakayokupeleka kwenye ndoto uliyonayao.

## NDOTO NI NINI? [What is Dream]

***Dream is a mental Image that shows how your future could be.*** Ndoto ni ile Picha iliyopo kwenye ufahamu wako inayoonyesha ni namna gani unataka maisha yako ya baadae yawe. Kwa mfano kuna watu ambao wanapenda kuwa Madaktari, Marubani, Waalimu, Wahasibu au Wanasheria hii ndio ndoto yao. Ni kile wanachotamani wasome mpaka wakifikie.

***Wewe Ndoto yako ni Nini? [Unataka kuwa nani baadaye?]***

Mimi…………........................................................
nataka kuwa……………………………….............

KiBiblia kama hauna ndoto, malengo au maono juu ya maisha yako ya baadae ni rahisi sana kuwa mzembe, mvivu, mhuni na mwanafunzi asiyejielewa shuleni, Angalia;

*"Pasipo na maono watu huacha kujizuia; …………"*
*Mithali 29:18.*

Kwa hiyo ikiwa utaingia sekondari na kuanza kusoma bila malengo au ndoto ni rahisi sana kujikuta unakwenda kinyume na kilichokupeleka Shuleni.

Ni hakika kwamba **NDOTO** au **MALENGO** uliyonayo ni lazima yatimie. Biblia inasema iandike hiyo ndoto na fanya bidii huku ukiendelea kuisubiri nayo ni lazima itimie. Ile nafasi pale juu uliyoijaza imeonyesha dhahiri ndoto uliyonayo, na mimi sasa kwa kukusaidia nitakuonyesha masomo na michepuo ya kuzingatia sekondari ili ufikie ndoto yako.

## MICHEPUO/TAHASUSI [Combination]

Unapofanikiwa kwa kiwango cha kufaulu kidato cha Nne Kwenda Kidato cha Tano, mfumo wa kusoma hubadilika. Kwa mfano badala ya kusoma masomo yote kama awali utasoma kwa mfumo unaoitwa Tahasusi zamani Mchepuo [Combination]. Kuna tahasusi/michepuo mbalimbali ya masomo ya Sayansi na masomo ya Sanaa, masomo ya Uchumi na Biashara, Masomo ya Kilimo n.k

Kila tahasusi moja huwa na masomo matatu tu. Hebu angalia hili jedwali hapa chini la michepuo mbalimbali ya masomo.

## MICHEPUO YA SAYANSI

| MCHEPUO | MASOMO | NDOTO/ MALENGO/ UTAALAMU |
|---|---|---|
| **PCM** | Physics, Chemistry, Mathematics | Wahandisi, Wafamasia, Wahasibu, Wanauchumi, Wataalam wa Takwimu na Hesabu, Walimu |
| **PCB** | Phsics, Chemistry, Biology | Madaktari wa Binadamu, Madaktari wa Wanyama, Watafiti wa Sayansi, Walimu |
| **PGM** | Physics, Geography, Mathematics | Marubani, Wataalamu wa madini, Wataalam wa Jiografia, Wanauchumi, Walimu |
| **CBG** | Chemistry, Biology, Geograph | Wataalamu wa Nyanja mbalimbali za kisayansi, Mazingira, Wanyama na Mimea, Walimu |

# MICHEPUO YA SANAA

| MCHEPUO | MASOMO | NDOTO/ MALENGO/ UTAALAMU |
|---|---|---|
| **HGL** | History, Geography, English Language | Wanasheria, Wanasiasa, Wanasaikolojia, Walimu wa lugha, Wataalamu wa Historia |
| **HGK** | History, Geography, Kiswahili | Wanasheria, Wanasiasa, Wanajiografia, Walimu n. k |
| **HKL** | History, Kiswahili, English Language | Wataalamu wa Lugha, Wanasiasa, Wanadiplomasia, Walimu n.k |

# MICHEPUO YA UCHUMI NA BIASHARA

| MCHEPUO | MASOMO | NDOTO/MALENGO/ UTAALAMU |
|---|---|---|
| **EGM** | Economics, Geography, Mathematics | Wanauchumi, Wahasibu, Maafisa masoko na wafanya biashara |

| | | |
|---|---|---|
| **HGE** | History, Geography, Economics | Wanauchumi, Wahasibu, maafisa masoko, Waalimu na Wafanya Biashara |
| **ECA** | Economics, Commerce, Accounts | Wanauchumi, Maafisa Masoko, Wahasibu, Wafanya Biashara |

# MICHEPUO YA KILIMO

| MCHEPUO | MASOMO | NDOTO/ MALENGO/ UTAALAMU |
|---|---|---|
| **CBA** | Chemistry, Biology, Agriculture | Wataalamu mbalimbali wa kilimo na mifugo |

# MAMBO YA KUZINGATIA

1. Ni muhimu sana kwa wakati huu kusoma masomo yote kabisa kwa bidii kubwa mpaka utakapohitimu Kidato cha Nne, Hii itakusaidia kupanua uwigo wa Kufaulu.
2. Zingatia mno ninasisitiza kujifunza juu ya mchepuo wa masomo yatakayokupeleka kwenye Ndoto yako.
3. Tafuta washauri sahihi ambao walishasoma unachotarajia kusoma ili wakuongezee mbinu

thabiti za kuifikia ndoto yako.

4. Andika mahali ndoto yako na usiache kuiombea mara kwa mara, shirikisha marafiki wazuri na watu sahihi ndoto yako ili wakutie Moyo na kukuombea pia.
5. Kumbuka kuna baadhi ya kazi au utaalamu unaweza kufikia kwa kusoma mchepuo wowote mfano Uaskari.
6. Si kila mchepuo nimeandika kazi au utaalamu wake mpaka mwisho, Hivyo baadhi ya mambo utaendelea kuyafahamu zaidi kadiri unavyoendelea kusoma.
7. Ni muhimu kuzingatia ushauri wa walimu, wazazi na washauri mbalimbali kulingana na uwezo ulionao wa masomo fulani na ndoto yako.

SURA YA 4

# MAMBO 7 YA MSINGI YA KUZINGATIA SHULENI

Ili ufanikiwe vizuri unapokua shuleni ni muhimu sana kuzingatia mambo haya saba ya msingi na muhimu kama ambavyo nitakuelekeza. Wanafunzi wengi wa sekondari wamekua wakifeli sana na hata kukata tamaa ya shule na maisha kwa sababu tu ya kutokuzingatia haya mambo. Na ninaomba sana uelewe kwamba unatakiwa kuyazingatia yote saba kama inavyotakiwa na si tofauti na hapo. Mambo hayo saba ni kama yafuatayo: -

## 1. TAALUMA

Ni dhairi na kila mmoja anatambua kwamba jambo kubwa na la msingi ambalo limekufanya uwepo shule ni kusoma na si tofauti na hapo. Hatuendi shuleni kukua, hatuendi shuleni ili kula, hatuendi shuleni kutafuta wachumba, hatuendi shuleni kucheza, hatuendi shuleni kuoga ila tunaenda shuleni ili **TUSOME** tupate maarifa na mwisho wa siku **TUFAULU.**

Nimedhamiria kukusaidia kwa kina juu ya namna, mbinu na mikakati mbalimbali itakayokusaidia kufaulu unapokua shuleni. Ukizingatia mbinu hizi ninakuhakikishia kufaulu kwako na kusonga mbele.

Hapo nyuma nilikufundisha juu ya masomo mbalimbali yanayofundishwa sekondari, lakini pia nilikufundisha juu ya ndoto yako inavyohusiana na masomo husika ili uifikie. Sasa kaa mkao mzuri wa kuelekezwa namna ya kusoma, kufanya mitihani na mpaka unachotakiwa kufanya baada ya mitihani.

## MTAJI MKUBWA KABISA KWAKO NI BIDII.

***"…………A man reaps what he sows"***
***"…………mtu huvuna alichopanda"***
***Wagalatia 6:7***

Ni lazima ukubaliane na andiko hili kwamba kwa namna yoyote ni lazima uvune tu ulichopanda na si tofauti na hapo. Unapokuwa shuleni ukipanda bidii na jitihada utavuna KUFAULU VIZURI, lakini pia ukipanda Uvivu na Uzembe utavuna KUFELI. Na hii ni kanuni ya kiMungu na haijalishi unaomba kiasi gani au unasoma Neno [Biblia] kiasi gani.

**Bidii ni kule kufanya jitihada na kazi kwa bidii bila kukata tamaa wala kuzembea.**

**Diligence is all about making an effort, working hard and tight.**

***Mithali 12:24 "Mkono wa mwenye bidii utatawala; ."***

Unapofanya bidii uwe na uhakika utafanikiwa kwa kiwango kizuri sana. Hivyo anza sasa kuchagua bidii iwe sehemu muhimu ya maisha yako ya shule na kamwe hutojuta.

Bidii yoyote ni lazima iambatane na maarifa, kwa maana bidii tu bila maarifa ni sawa tu na kupoteza nguvu kubwa huku unasukuma ukuta ambao mwishoni utachoka na hakuna chochote kitakachoonekana umefanya.

***Warumi 10:2 "..............lakini juhudi yao haina maarifa."***

Ni vizuri tu pia ufahamu ni gharama kufanya bidii, si kitu kirahisi bali ni kitu kinachohitaji uumie, ujitoe na uwe tayari kupoteza baadhi ya mambo uyapendayo tena kwa kutokujionea huruma hata kidogo. Lakini

pia bidii inakuhitaji uwe na msimamo binafsi wa kutokuendeshwa na kitu kingine chochote wakati ambao unatakiwa ufanye unachotakiwa kufanya. Na ndio maana kwenye kusoma pia ni lazima ufanye bidii kubwa tena yenye maarifa. Na tunachokupa hapa ni mbinu za kuwa na bidii yenye maarifa ndani yake.

***"Let laziness be your worst enemy and hardwork your best friend"*** **Theodore Roosevelt.**

**Zaburi 126:6** ***"Ingawa mtu anakwenda zake akilia azichukuapo mbegu za kupanda. Hakika atarudi kwa kelele za furaha, aichukuapo miganda yake."***

## MBINU ZA KITAALUMA ZENYE BIDII YENYE MAARIFA

### MAMBO YA KUFANYA DARASANI;

- Ingia darasani mapema zaidi au kwa muda uliopangwa.
- Msikilize mwalimu kwa makini, na fanya mazoezi yote mnayoachiwa tena kwa muda.
- Fahamu ratiba ya masomo ya darasani, hii itakusaidia kujiandaa vizuri.
- Fahamu mitaala (syllabus) kwa masomo yote

katika ngazi yako itakusaidia kuwa makini.

- Rudia kusoma kile mlichofundishwa, pale ambapo hujaelewa tafuta msaada aidha kwa wanafunzi wenzako au mwalimu.
- Hakikisha unakaa sehemu nzuri darasani isiyo na usumbufu na utakayomsikia mwalimu vizuri. Pia jenga tabia ya kujibu maswali darasani bila woga, pia kumuuliza mwalimu pale ambapo haujaelewa.
- Epuka kutokatoka darasani wakati mwalimu anapofundisha maana hii itakuondolea umakini wa kuelewa vizuri kile anachofundisha, tumia muda wa mapumziko kwenda uani na kufanya mambo yako mengine ila kamwe isiwe muda wa darasani.
- Jenga tabia ya kumpenda mwalimu wa somo, kulipenda somo husika hata kama ni gumu kwako, hii itajenga fikra chanya ndani yako na kufungua ufahamu na uelewa wako.
- Sikiliza kwa umakini mkubwa mada yoyote inayotolewa hata kama ulishaisoma kabla, Isikilize kwa makini kama vile haukuwahi kufundishwa hiyo mada kabla, hii itaongeza uelewa wako wa kina kabisa kwenye mada husika.

## MAMBO YA KUFANYA UNAPOJISOMEA MWENYEWE;

- Hakikisha una ratiba binafsi iliyopangwa vizuri ya kujisomea binafsi, Uliyopanga kwa muda na yenye masomo yote.
- Jifunze kusoma kwa mfumo wa kuandika, yaani unasoma kisha unaandika kile ulichokielewa, kumbuka asilimia kubwa ya mitihani hufanywa kwa kuandika. Na unapoandika mara nyingi itakusaidia kukamata vizuri ulichokiandika pamoja na kutokosea herufi za maneno husika {Spellings}.
- Ni vizuri kujifunza kuandika pointi na maeneo muhimu ya mada au somo husika kwa ufupi (SUMMARY), hii itakusaidia kukukumbusha kwa ufanisi. Lakini pia itakusaidia kusoma kwa urahisi ukiwa eneo lolote bila hata madaftari.
- Ni muhimu sana uwe na kundi la kujadiliana mada mbalimbali za kimasomo (GROUP DISCUSSION), Hakikisha kundi lako lina watu makini wanaopenda kusoma, kufaulu na wenye malengo makubwa na wanaojali muda.

## MAMBO YA ZIADA YA KUFANYA;

- Jenga tabia ya kununua vitabu na vitini vya masomo mbalimbali pamoja na kudurufu (Photocopy) mitihani iliyopita (Past Papers), kisha visome kwa bidii na umakini mkubwa.

- Pale inapohitajika nenda TWISHENI inaweza kukuinua, Zaidi jifunze kwenda TWISHENI, za uhakika hata kama ni gharama. Kumbuka ni walimu wa shule chache sana wenye uwezo wa kumaliza mitaala kwa wakati, ninakuonya tena usiende twisheni kishabiki, nenda TWISHENI ukiwa unajua unakwenda kusoma masomo yapi na mada (Topics) zipi.
- Jenga urafiki na wanafunzi wa shule zingine, hii itakusaidia kupata mwanga mkubwa juu ya njia mbalimbali wanazotumia wao lakini pia mtasaidiana kwenye masomo na kubadilishana matirio.

## MAMBO YA KUFANYA KUELEKEA MITIHANI;

- Hakikisha mnajadiliana kwa kina mitihani yote ya nyuma (Past Papers).
- Fanya mitihani yote ya kabla ya mitihani ya mwisho kwa mfano Mock na PRE – NATIONAL bila kudharau, hii itakusaidia kujua uhalisia wa kiwango chako, pia itakusaidia kurekebisha makosa uliyonayo na itakuandaa kufanya vizuri kwenye mitihani ya kitaifa.
- Kamwe usifikirie kutegemea kuvuja kwa mitihani, kusaidiwa au kuingia na udanganyifu wowote kama vibuti n.k. Mawazo haya yatakusababishia kufeli vibaya mno.

- Jiamini juu ya kile ulichosoma na unachojua, tumia muda uliobaki kurudia na kurudia kujisomea kwa bidii, hii itapunguza uoga na kuongeza kujiamini kwako.

## MAMBO YA KUFANYA KIPINDI CHA MITIHANI;

- Kipindi cha Mitihani fahamu ratiba ya mitihani yako mapema sana na ikiwezekana ikishabandikwa iandike mahali na anza kujisomea kwa mujibu wa ratiba yako. Hii itakurahisishia kuendana na mazingira ya maandalizi ya mwisho kuelekea mitihani.
- Siku za mitihani amka mapema jiweke wakfu kwa Bwana ukihitaji ulinzi, ujasiri na ukumbusho wa Roho Mtakatifu kisha anza kukiri ushindi, kufaulu na kusonga mbele.
- Hakikisha unafika mapema kwenye chumba cha Mtihani, kwa mujibu wa sheria ni nusu saa kabla ila kwako hata saa moja kabla uwe karibu na chumba cha mtihani.
- Ondoa hofu na uoga wa maaskari na wasimamizi wa mitihani maana hao hawana cha kufanya juu ya kuandika kwako mtihani, unahitajika kuwa mwaminifu tu.
- Kamwe usiwe na haraka ya kufungua mtihani, kaa kwa utulivu ukiutafakari ukuu wa Mungu huku ukisikiliza maelekezo ya wasimamizi wa

Mitihani kwa makini.

- -Mshukuru Yesu kimya kimya kwa msaada wake katika mtihani huo kisha ufungue na soma maelekezo ya awali kabla haujafanya chochote, kisha pitia maswali yote na baada ya hapo anza kujibu mtihani wako ukianza na yale maswali ambayo yatakuwa ni marahisi zaidi kwako na yanabeba alama au maksi nyingi zaidi.
- Epuka kukatakata au kuchafua karatasi yako ya kujibia mtihani, amini katika Mungu na uwezo wako wa kujibu huo mtihani, hakikisha unatumia muda vizuri kama ulivyopangwa.

## MAMBO YA KUFANYA BAADA YA MITIHANI;

- Hata kama mtihani utakuwa mgumu kiasi gani epuka kuongeaongea maneno hasi kama JAMANI WAMETUUA, HIVI TUTAFAULU KWELI, IMEKULA KWANGU HII, MTIHANI UMENIONA, Maneno yako ni Uhai na Yanaumba lolote utakalozungumza, hivyo epuka kabisa haya, AMINI katika Uweza wa Mungu na epuka sana kujadilijadili mtihani mliotoka kufanya badala yake hamishia nguvu zako kwenye mitihani inayofuata.

- Endelea kuombea mitihani yako hata baada ya kumaliza ili Ulinzi wa Mungu uwepo kwenye usahishwaji wa mitihani yako, upangaji wa matokeo na hatimaye kupokea matokeo, KIRI USHINDI, KUFAULU, KUSONGA MBELE.

## 2. MARAFIKI

Unapokua shuleni moja kati ya mambo muhimu sana ya kuwa nayo makini ni aina ya marafiki wa kuambatana nao. Aina ya marafiki ulionao wanaweza kuamua kufanikiwa au kufeli kwako.

Mtu mmoja alisema **"NIONYESHE MARAFIKI ZAKO NAMI NITAKWAMBIA ULIVYO",** Unajua ni kwanini alisema hivyo? Ni kwa sababu mara zote watu wenye tabia na mwenendo mmoja mara nyingi sana wanashibana na kuambatana kuwa marafiki. Marafiki wana uwezo mkubwa sana wa kukuambukiza tabia, mwenendo na mitazamo yao. Ndio maana Neno la Mungu kwenye kitabu cha Suleimani cha Mithali anasema;

***"Usifanye urafiki na mtu mwenye hasira nyingi; Wala usiende na mtu wa ghadhabu nyingi; Usije ukajifunza njia zake; Na kujipatia nafsi yako mtego" Mithali 22:24-25.***

Hii inakusaidia kutambua nguvu ama uwezo walionao marafiki katika kukubadilisha na kukufanya uishi kama wao au uwe kama wao.

***"Mwanangu, wenye dhambi wakikushawishi, Wewe usikubali"***
***Mithali 1:10***

Unachotakiwa kufanya unapoingia shuleni usikurupuke kumpa mtu nafasi ya kuwa rafiki yako wa karibu kabla haujamtambua vizuri, epuka sana kukurupuka kuchagua marafiki hasa wale waliokutangulia shuleni bila kutambua kwa kina tabia zao na namna tu walivyo.

Muombe sana Mungu akukutanishe na marafiki sahihi kwenye shule yeyote utakayoenda kusoma, Mungu akupe marafiki wenye upendo wa dhati na moyo wa kukubeba na kukuelekeza ili ufikie hatma njema ya malengo na ndoto ulizonazo. Unahitaji marafiki wanaojua kilichowaleta shuleni na wanakifanyia kazi, wenye hofu ya Mungu {wanaouchukia uovu} na wenye upendo wa kweli kwako na si tofauti na hapo.

# 3. WALIMU

*"Mwanafunzi na amshirikishe mwalimu wake katika mema yote"*
*Wagalatia 6:6*

Biblia inaweka wazi kwamba mwanafunzi na amshirikishe mwalimu wake katika mema yote, ni muhimu sana kuwa na mahusiano mazuri na sahihi na walimu wako ili ufanikiwe katika masomo yako na mambo mengine muhimu shuleni. Nimewahi kuwaona wanafunzi wengi sana waliokuwa na uwezo mkubwa wa darasani kimasomo ila walifeli mwisho wa siku kwa sababu tu walikuwa na mahusiano mabaya na walimu wao.

Ni muhimu sana utambue kwamba WALIMU ndio wazazi na walezi wako unapokua shuleni. Na ni dhairi zipo baraka nyuma ya kuwapenda na kuwaheshimu walimu wako, lakini pia ipo laana nyuma ya kutowapenda na kuwadharau walimu wako. Kila mara ninapokutana na wanafunzi huwa ninawasisitiza sana kuwaheshimu na kuwapenda walimu wao hata kama huwa hawawaelewi darasani ama huwa ni wakali sana.

Mwalimu yeyote duniani anapenda kuheshimiwa na kusikilizwa na wanafunzi wake kwa bidii, anapenda kuombwa ushauri na msaada na mwanafunzi wake. Walimu wote huwapenda wanafunzi wenye nidhamu na utii wa kutosha tena usio wa kuigiza. Anza sasa kujenga mahusiano sahihi na walimu wako wanaokufundisha sekondari kwa kuwapenda, kuwatii na kuwaheshimu. Washirikishe juu ya mema na changamoto mbalimbali unazopitia kwenye masomo na maisha ya shuleni kwa ujumla. Na mwisho wa mambo yote utaona matunda mazuri yaani mafanikio ya mahusiano mazuri na walimu wako.

## 4. DINI

***"Mkumbuke Muumba wako siku za Ujana wako............." Mhubiri 12:1***

Karibu shule zote zina ratiba ya kueleweka ya vipindi vya dini. Lakini pia karibu shule zote zina vikundi mbalimbali vya dini ambavyo vinawakutanisha wanafunzi wa imani moja kumwabudu Mungu kwa pamoja, kwa mujibu wa taratibu na muongozo wa kikundi au dini husika.

Jambo la kwanza la msingi unalotakiwa kujua na nililieleza sana mwanzoni, ni kwa habari ya nafasi na umuhimu wa Mungu kwenye masomo yako na maisha yako ya shule kwa ujumla. Serikali kupitia wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi wanalitambua hili, na ndio maana wakakubaliana na kuamini kuruhusu vikundi na vipindi vya dini viwepo mashuleni. Hivyo kukataa na kudharau kuingia vipindi na vikundi vya dini NI SAWA na kukataa nafasi na msaada wa Mungu kwenye masomo na maisha yako kwa ujumla.

## JE! VIKUNDI HIVYO NI VIPI na MIMI NINATAKIWA KUINGIA KIKUNDI GANI?

Utakapofika shuleni utakutana na vikundi mbalimbali na utajiunga kwenye kikundi kulingana na dhehebu la Kikristo unalotoka linalohusiana na hicho kikundi: -

### i]. **KIKUNDI CHA UKWATA.**

Hiki ni kikundi kinachowaunganisha wanafunzi wote wanaotoka makanisa yaliyopo chini ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania {CCT} ambayo ni KKKT, Anglikana, Kanisa la Mungu, Moravian, BAPTIST, AIC, na mengineyo ya CCT. Kama unatoka kwenye hayo madhehebu ukifika shuleni utajiunga

na kikundi kinachoitwa **UKWATA** ili umwabudu Mungu na kuijenga imani yako pamoja na wenzako. Shirikiana nao kwa kila kitu.

ii]. **KIKUNDI CHA TYCS.**

Hiki ni kikundi kinachowaunganisha wanafunzi wa sekondari toka dhehebu la **ROMAN CATHOLIC[RC],** Hivyo kama unatoka dhehebu la RC ni muhimu kujiunga na kikundi hiki.

iii]. **KIKUNDI CHA CASFETA.**

Hiki ni kikundi cha wanafunzi wanaotoka madhehebu ya **Kipentekoste** wengi wanapenda kuyaita makanisa ya **kiroho** au ya **kilokole**. Hivyo kama unajifahamu kwamba unatoka katika moja ya hayo makanisa ya kiroho au ya kilokole hiki ni kikundi maalum na muhimu kwa ajili yako. Karibu na shirikiana na wenzako kwenye shule husika.

iv]. **KIKUNDI CHA ASSA.**

Hiki ni kikundi cha wanafunzi wote wanaotoka katika makanisa ya **Kisabato,** hivyo basi kama unatoka katika kanisa la Kisabato ni muhimu kujiunga na kikundi hiki, ili kumwabudu Mungu pamoja na wenzako.

HAKIKISHA KABISA UNAJIUNGA NA KIKUNDI HUSIKA maana KUPITIA HIVI VIKUNDI MAISHA YA WATU WENGI YA KIROHO NA KITAALUMA YAMEBADILISHWA NA KUFANYWA BORA NA YA MAFANIKIO. Na Mimi ni Moja kati ya hao watu.

## 5. USAFI

***"Mtu awaye yote asiudharau ujana wako bali uwe kielelezo katika........usafi...." 1 Timotheo 4:12***

Moja kati ya mambo muhimu sana unapokua shuleni ni USAFI, hii ni kwa wanafunzi wanaosoma KUTWA na BWENI. Kwa wale wanaosoma BWENI ndio haswa inabidi wajitambue kwamba wanatakiwa kuwa wasafi maana hakuna mtu wa kuwasimamia kwa karibu kama wale ambao wanaosoma kutwa, ambao wazazi wanaweza kuwasimamia bado. Hakikisha unakua mfano wa kuigwa wa usafi kwenye darasa na hata shule yako.

### i]. USAFI BINAFSI

Huu ni usafi wa mtu mwenyewe ambao huusisha usafi wa mwili wake, nguo anazovaa, malazi yake na vyombo anavyotumia kwa ajili ya chakula. Usafi

huu ni muhimu sana uzingatiwe na kila mwanafunzi maana una faida kubwa sana kwako kiafya na kimasomo. Hebu hakikisha mambo yafuatayo yanafanyika sehemu muhimu ya maisha yako: -

- Kuoga kila siku walau mara moja.
- Kufua nguo zako za ndani kila siku.
- Kupiga meno mswaki walau mara mbili kwa siku au kila baada ya kula.
- Hakikisha sare zako za shule zinakua safi kila wakati pamoja na soksi.
- Hakikisha unakata kucha zako kila wakati.
- Zingatia usafi na urefu wa nywele zako.
- Mashuka na kitanda hakikisha vinakua safi na kutandikwa vizuri kila siku.
- Hakikisha unaosha vyombo unavyotumia kwa chakula kila unapomaliza tu kula na vihifadhi sehemu salama.

## II]. USAFI WA MAZINGIRA

- Hakikisha unawajibika ipasavyo juu ya eneo lolote utakalopangiwa kufanya usafi.
- Epuka tabia ya kutupa uchafu hovyo au kukojoa maeneo yasiyo sahihi.
- Hakikisha unatumia vyoo na mabafu vizuri na kistarabu.
- Ni vizuri kuyapenda mazingira yote unayoishi

maana kuna faida kubwa kwenye usafi.

**UMUHIMU WA USAFI**

- Usafi hutuepusha na magonjwa ya namna mbalimbali na hasa yale ya mlipuko.
- Usafi hukufanya mwepesi na kufungua ufahamu wako kila wakati.
- Usafi hukujengea Ujasiri mbele za watu pamoja na kujiamini.
- Usafi hufanya watu wakupende na wakuheshimu.
- Usafi hukusaidia kusoma bila woga wala wasiwasi wa aina yoyote.

**KINYUME NA HAYA NDIO HASARA au MADHARA YA KUWA MCHAFU, CHAGUA SASA KUWA MSAFI KILA WAKATI SAWASAWA NA MAELEZO HAYA MAZURI YA USAFI.**

## 6. MICHEZO

Moja ya mambo muhimu ya kujihusisha nayo unapokua shuleni ni michezo. Hakikisha una michezo walau miwili unayojihusisha nayo kwa bidii zote. MICHEZO inaweza ikawa ni ile ya kutoa jasho jingi kama kukimbia, kuruka juu au chini, kucheza

aina yoyote ya mpira iwe ni wa kikapu, miguu, pete, wavu au mikono, LAKINI pia inaweza kuwa ni kurusha tufe, mkuki na mengineyo mingi. AINA nyingine ya michezo ni ile ambayo huwa haitutoi jasho kama Kuigiza, kucheza ngonjera, kuimba, na inayofanana na hii.

Msisitizo wangu ni Wewe kujihusisha walau na aina moja ya mchezo wa kutoa jasho na aina moja ya michezo isiyotoa jasho. Ni muhimu sana kucheza ukiwa shuleni maana michezo ina faida kubwa sana kwenye masomo, afya na maisha yako kwa ujumla.

## FAIDA ZA MICHEZO

- Michezo hukufanya mkakamavu kila wakati na huondoa uzembe na udhaifu.
- Michezo hulinda mwili dhidi ya magonjwa kwa kutengeneza kinga ya mwili.
- Michezo hujenga urafiki baina ya wahusika ambao hukutana kwenye hiyo michezo.
- Michezo hutusaidia kujifunza maeneo mapya na kufahamiana na watu wapya.
- Michezo hudumisha umoja miongoni mwa wahusika wa Timu moja au eneo moja.
- Michezo huibua vipaji na vipawa mbalimbali walivyonavyo wahusika mbalimbali.
- Michezo hutuletea TUZO na hata PESA na

hasa kwenye mashindano makubwa.

NI MUHIMU SANA USHIRIKI KWENYE MICHEZO wakati wa vipindi vya michezo unapokua shuleni tena bila kukosa.

## 7. ADABU NA MISIMAMO BINAFSI

***"Maneno ya kinywa changu, Na mawazo ya moyo wangu, Yapate kibali mbele zako. Ee BWANA"***
**Zaburi 19:14**

**ADABU** ni kufanya unachotakiwa kufanya hata kama hautaki ili uweze kufikia lengo flani.

***Waebrania 12:7 "Vumilieni taabu kwa ajili ya kufunzwa adabu….."***

Moja ya mambo muhimu sana shuleni ni kuwa na adabu, nidhamu na heshima kwakila mtu, kuanzia walimu, viongozi wa wanafunzi [Viranja] na hata wanafunzi wenzako.

Hii ni moja ya nguzo za msingi zitakazokusaidia kuishi shuleni kwa amani, furaha tenabila kubughudhiwa wala kusumbuliwa.

Ili uishi shuleni kwa amani ni muhimu sana kuishi sawasawa na sheria za shule.

Sheria za shule ndiyo muongozo wako wa maisha ya shule na si vinginevyo. Ni lazima uishikama sheria za shule zinavyoelekeza hata kama kuna baadhi ya sheria huzipendi. Biblia inasema vumilia taabu kwa ajili ya kufunzwa adabu.

## NGUZO ZA KUKUSAIDIA KUWA NA ADABU na MSIMAMO BINAFSI.

1. Kila wakati uwe na fikra au mawazo chanya juu yako na hata juu ya wengine. Fikra zako ndio maisha yako, chochote unachofikiri ndicho hutokea, ndio maana Biblia inasema;

**" .... AFIKIRIVYO MTU NDIVYO ALIVYO"**
***Mithali 23:7***

2. Thamini na heshimu kila mtu, unayemjua na usiyemjua, mkubwa kwa mdogo.
3. Jenga mfumo sahihi wa kuwasiliana, Jifunze kuzungumza na watu kulingana na rika zao. Kuna tofauti kubwa ya namna unavyoongea na mwanafunzi mwenzako na utakavyoongea na mwalimu wako.
4. Changamana ipasavyo kila wakati na wanaokuzunguka katika mema yote.
5. Fanya unalopaswa kufanya hata kama haujisikii kufanya,
6. Jifunze kuongea maneno chanya na ya

kufanikiwa kuhusu Wewe binafsi na watu

7. Wengine, maana maneno yanaumba na ipo nguvu katika vinywa vyetu. Chochote
8. Unachoongea mara zote ndicho kinachotokea.
9. Kamwe usiendeshwe na matukio au mambo ya marafiki au ya darasa yasiyoeleweka. Simamia ndoto yako na sheria za shule kwa uaminifu hata kama watakuona mjinga.
10. Weka wazi misimamo yako juu ya nini hautafanya na kipi unafanya ili watu wakuelewe vizuri, hata kama mwanzoni watakucheka na kukudharau ila ipo siku watakuelewa na utaishi maisha mazuri sana.
11. Achana na mambo ya urafiki uliopitiliza wa kushirikiana kila kitu, wapo ambao waliingia shuleni wakakutana na marafiki wajanja wakashirikiana mpaka matumizi waliyopewa nyumbani na walipoishiwa vya kwao marafiki waliwakimbia.
12. Kamwe usizidishe uzito kwenye jambo lolote bali kila jambo lifanyike kwa wakati wake, kwa mfano wakati wa darasani ingia darasani, wakati wa kujisomea jisomee, wakati wa dini ingia mwabudu Mungu katika roho na kweli, wakati wa kupumzika pumzika, na wakati wa kulala lala usipige hadithi.

**"MKIYAJUA HAYA HERI NINYI MKIYATENDA"**

SURA YA 5

# MAKOSA MAKUBWA 18 YANAYOSABABISHA WENGI KUFELI

***"Aonywaye mara nyingi akishupaza shingo, atavunjika ghafla, wala hapati dawa." Mithali 29:1***

***"Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu; lakini mwisho wake ni njia za mauti." Mithali 16:25***

Yapo makosa ya namna mbalimbali ambayo wanafunzi wengi huyafanya wanapokua shuleni na hii imewagharimu wengi na kujikuta wanafeli na kupoteza dira na ndoto za maisha yao. Wapo ambao walionywa na kushauriwa sana lakini hawakusikia, wapo ambao walipewa mpaka adhabu lakini mwisho wa siku waliendelea na makosa yao.

Tunakufundisha juu ya haya makosa ili hii ikusaidie kuyaepuka na ikupe umakini wa kusonga mbele.

**KOSA LA 1: Kutokubaliana na mazingira ya shule na kulalamika kila siku.**

Wapo wanafunzi wengi wanaofeli wakilalamika shule haina waalimu, vitabu, maji, na wengine pia husema hawana waalimu wazuri hivyo wanaacha kufanya bidii ya masomo. Hata sisi tulisoma shule kama hizo ila bidii yetu ndiyo iliyotufanikisha hivyo na wewe pia fanya bidii kwa kila hali unayokutana nayo shuleni bila kulalamika.

**KOSA LA 2: Kuchagua masomo mapema, napenda hili na sipendi hili.**

Wanafunzi wengi waliofeli ni wale waliochagua masomo mapema na wengine kujikuta wamechagua masomo ambayo hawayawezi na mwishowe wakaishia kufeli. Tunakushauri soma masomo yote kwa bidii sana na matokeo yake ndiyo yatakayokufanya uchague masomo unayo elewa zaidi na kufanya vizuri darasani.

**KOSA LA 3: Kufata mkumbo kwa waliotangulia shuleni tena wasiojielewa.**

Wanafunzi wengi wamepoteza dira na mwelekeo

wa masomo yao kwa sababu ya kufuata ushauri toka kwa watu wazembe waliofeli, wanabaki kuambiwa eti Hesabu ni ngumu, Physics ni Ngumu, Chemistry ni Ngumu na mengine mengi, nao wakaacha kusoma hapo ndo kukawa mwisho wa mafanikio yao. Ndio maana nimekuandikia hiki kitabu mdogo wangu mambo yote shuleni ni marahisi sana ukiyafanyia bidii na Mungu akusaidie.

**KOSA LA 4: Kujiingiza kwenye mahusiano ya kimapenzi mapema.**

Hili ndilo kosa ambalo wanafunzi wengi wakishalifanya ni lazima apunguze kasi ya kufanikiwa akiwa shuleni. Ninakushauri sana tena sana usijaribu kujiingiza kwenye mahusiano ya Kimapenzi ukiwa shuleni kwani umeenda shuleni kusoma. Pia muda ulionao wa kusoma ni mdogo sana usiupoteze.

**KOSA LA 5: Kutoandika notes papo hapo na kusubiri kuandika baadaye.**

Unapochelewa kuandika notes mwalimu anapofundisha utakuwa umepoteza kumbukumbu kubwa sana kwani mwalimu anapofundisha na wewe kuandika notes muda ule, unajipa uwezo mkubwa wa kuja kuyakumbuka yale uliyoyaandika kwa mapema

zaidi kuliko kuandika baadaye, pia itakusaidia kutunza muda wako.

**KOSA LA 6: "COPY PASTE" ya mazoezi mbalimbali yanayoachwa na mwalimu.**

Mwalimu anapoacha maswali anataka kila mwanafunzi ayafanye na kwa Yule atakaye shindwa akamuulize mwalimu au akamuulize rafiki yake jinsi ya kufanya na sio kukopi kazi aliyofanya mwanafunzi mwingine. Hii itakusaidia kukumbuka maswali na jinsi ya kujibu.

**KOSA LA 7: Kujing'ang'aniza kwa marafiki wabaya na wasiojielewa.**

Hakuna shule isiyokuwa na wanafunzi wenye tabia mbaya, ila ni jukumu lako wewe unayesoma kitabu hiki kuangalia ni marafiki wapi wa kushirikiana nao kwenye mambo yako unayofanya hasa ya Kimasomo na Kimichezo.

**KOSA LA 8: Migogoro na walimu, na kukwepa vipindi.**

Kwa mwanafunzi yeyote aliyejaribu kufanya hili kosa hana namna ya kufanikiwa tena kimasomo kwani

Walimu na Vipindi darasani ndio NGUZO kuu ya mwanafunzi yeyote kufaulu, hivyo usijaribu au kushirikiana na wanafunzi wa namna hii.

**KOSA LA 9: Kujihesabu uwezo wa kimasomo ambao hauna.**

Wanafunzi wengi wanapenda kuishi kwa mazoea eti kwa sababu alikuwa anaongoza akiwa Elimu ya Msingi anapoingia Elimu ya Sekondari hafanyi bidii ya masomo akififikiri mambo yatakuwa sawa na kule, na hapo ndipo unapokuwa mwisho wake kimasomo. Tunakushauri sana usifanye kosa hilo. Umeenda shuleni kusoma hivyo soma bila kuwa na sababu yoyote na Mungu akutangulie.

**KOSA LA 10: Kujiwekea malengo rahisi na ya chini.**

Wanafunzi wengi waliojiwekea malengo rahisi sana wanakuwa hawafanyi bidii katika masomo yao, na hivyo kuwa wanafunzi wa kawaida sana wanaopata alama za chini sana na kushindwa kuendelea mbele. Wewe unayesoma hiki kitabu usiwe na malengo marahisi ili uwe unafanya bidii katika masomo yako kwani kila kitu kinawezekana. Nuia kupata ufaulu wa juu alama A kwa kila somo, hii itaamsha morali

ya kusoma kwa bidii ndani yako.

**KOSA LA 11: Kukesha kusoma usiku na kusinzia muda wa vipindi mchana.**

Hili kosa huwa wanafanya wanafunzi ambao wamepewa ushauri na watu waliokosa mwelekeo wa masomo yao, ila ninakushauri usome lakini pia upate muda mzuri wa kupumzika (Kulala) ili siku inayofuata uweze kuwa na nguvu pia uwezo wa kumsikiliza mwalimu darasani.

**KOSA LA 12: Kusikiliza na kuamini maneno ya wanafunzi waliotangulia.**

Hili kosa huwa linafanyika pale ambapo unapata muda wa kuwauliza maswali watu waliofeli au walioshindwa kusonga mbele kimasomo. Tunakushauri sana usijaribu kufanya kosa kama hili ila ukitaka kupata ushauri tafuta ushauri kwa watu waliofanikiwa sana kimasomo yaani wenye ufaulu mzuri wa masomo.

**KOSA LA 13: Kutoambilika na Ujuaji mwingi.**

Hili kosa huwa wanafanya hasa wanafunzi ambao wamekuwa wakifanya vizuri walipo kuwa Elimu ya Msingi hivyo wakitegemea kuendelea na staili ile

ile ya kusoma, na wanaposhauriwa na watu waliopo mbele yao kimasomo wanakuwa wabishi au wagumu kubadilika. Ninakushauri sana mdogo wangu kuwa mwepesi wakubadilika katika mambo mazuri na ya muhimu utakayokuwa unashauriwa.

## KOSA LA 14: Kusoma kipindi cha majaribio na mitihani tu.

Wanafunzi walio wengi huwa wanafanya hili kosa ila ni kwa sababu hawakupata mtu sahihi wakuwasaidia, ila usijaribu kupoteza muda wako kipindi cha masomo ya darasani bila kusoma ukijidanganya kuwa utasoma kipindi cha mitihani. Kipindi cha mitihani ni kipindi kigumu kwa kichwa cha mwanafunzi kushika vitu vipya vingi, hivyo kila muda uliopo shuleni toka shule inafunguliwa usiwe mtu wa kupoteza muda bali fanya juhudi sana katika kusoma kila siku ili wakati wa mitihani uwe unafanya kazi ya marudio kwa yale unayoyajua.

## KOSA LA 15: Kujitengenezea mibadala hewa i.e Nikifeli nafanya hivi na hivi.

Wanafunzi wengi wamepoteza dira ya masomo yao kwa kujiwekea mibadala hewa katika maisha yao mfano mwanafunzi anasema hata nikifeli nitakwenda

kuuza duka la mjomba. Usijaribu hata siku moja kujiwekea mibadala kama hii katika maisha yako. Kwani ndiyo itakayo kufanya usitie juhudi katika masomo yako.

## KOSA LA 16: Kuzidisha uzito upande mmoja i.e Dini, Michezo, Uongozi, Chakula.

Kuna mambo mazuri sana kila mwanafunzi anatakiwa ayafanye lakini kila jambo lina muda wake wa kufanya. Usifanye jambo lolote nje ya muda wake kama hamna ulazima wa kulifanya. Wanafunzi wengi wamekuwa wakitumia muda mwingi kwenye Michezo, Uongozi, Chakula na hata wengine Dini kiasi cha kuwafanya kuwa na muda kidogo wa kusoma na wakaishia kufeli hivyo. Ninakushauri usiwe mwanafunzi wa aina hii.

## KOSA LA 17: Kutotaka kushirikiana na wenzako kwenye masomo.

Wanafunzi wengi wanaogopa kujiunga na makundi ya kusoma wakijiona kama hawawezi au wana uwezo mdogo wa kushiriki na wenzio, lakini ninakutia moyo kwamba kila aliyepo shuleni anatakiwa kujifunza hivyo wewe unayesoma kitabu hiki hakikisha unapata kikundi cha kusoma na kujadiliana nacho masomo

unapokuwa shuleni kwani utaweza kujifunza mambo mengi, pia na wewe unaweza kusaidia wanafunzi wengine katika kundi lako kwenye eneo ulilo na uwezo nalo na Mungu atazidi kukubariki.

**KOSA LA 18: Kuumwa umwa hovyo shuleni kwa sababu ya uzembe tu na uvivu.**

Wanafunzi wengi wamekuwa wakitumia kauli ya KUUMWA ili wasishiriki vipindi mbalimbali shuleni au kazi mbalimbali shuleni. Ninakushauri sana mdogo wangu usifanye hili kosa kwani katika kushiriki vipindi au mambo mbalimbali kama michezo kuna mengi utajifunza ambayo yatakusaidia katika masomo yako.

SURA YA 6

# MISISITIZO THABITI-NGUZO KUBWA 10 ZA KUKUFANIKISHA

Jambo lolote ili lifike linapotakiwa kwenda ni lazima kuwe na nguzo muhimu za kushikilia jambo hilo ili lifike linapotakiwa kufika. Na Wewe kama mwanafunzi wa sekondari kuna mambo ambayo ni kama nguzo kwako ambayo yatakusaidia kufikia ndoto na malengo yako kwa kiwango kizuri. Ninaomba sasa ufatilie kwa kina ninapokuelekeza juu ya nguzo hizi.

## 1. PASSION/DESIRE/ READNESS

Hii ni nguzo ya kwanza muhimu sana ambayo ni SHAUKU, **UTAYARI** au **NIA YA NDANI** ya kutaka na kuamua kufanya jambo fulani. Ili uweze kufanikiwa shuleni ni lazima uwe na msukumo/ utayari na nia ya ndani ya kutaka kufaulu na kusonga mbele.

**JE UNA NIA NA UPO TAYARI KUFAULU?**

## 2. FOCUS

Nguzo ya pili ya msingi ni **KUJUA UNAPOKWENDA** na **NINI UNATAKA**, hii ni muhimu sana maana inakusaidia kupambana na changamoto zote. Ukijua unapokwenda hakuna cha kukubabaisha, hivyo hii ni nguzo kubwa sana.

**JE UNAJUA UNAPOKWENDA** na **NINI UNATAKA?**

## 3. COMMITMENT

Nguzo ya tatu ya msingi ni **KUJITOA KUFANYA KWA BIDII,** Unapojitoa kusoma kwa bidii na kwa kumaanisha, ni rahisi sana kufika unapotaka kwenda. Fahamu tu kwamba ni muhimu sana kujitoa kusoma kwa bidii bila kuangalia vikwazo wala vizuizi vyovyote.

**JE UPO TAYARI KUJITOA KUSOMA KWA BIDII?**

## 4. INTEGRITY

Nguzo ya nne ni **UADILIFU,** Hii ni kuishi kwenye uhalisia bila kujidanganya Wewe binafsi. **UADILIFU** ni ile hali ya maneno yako kuendana na matendo yako, yaani kuishi kile unachokizungumza

mbele za watu hata kama upo peke yako. Ukisema huwa unasoma sana, hakikisha unasoma sana hata kama hakuna mtu wa kuhakikisha hilo. Kamwe usijidanganye binafsi maana matokeo ya mwisho yatakuaibisha.

## 5. ACCOUNTABILITY

Nguzo ya tano ni **UWAJIBIKAJI,** Hii ni kule kuwa tayari kuwajibika pasipo kusubiri msaada wa mtu mwingine au kulalamika kivyovyote. Hakikisha unawajibika ipasavyo, kama ni jambo la kufanya fanya usisubiri wala usijiulizeulize. Na kivyovyote vile hakikisha jambo hilo linafanyika kwa wakati na kwa ubora pia.

## 6. EXCELLENCE

Nguzo ya sita ni **KUFANYA KWA UBORA,** Hii ni ile hali ya kupambana kufanya jambo kwa kina au kiwango cha juu kabisa cha uwezo wako. Kwa hiyo basi hakikisha kama ni kusoma kwa bidii, soma kwa kiwango cha juu cha uwezo wako na nuia kupata matokeo makubwa na bora zaidi kila wakati. Komalia kila wakati alama za juu kwenye masomo.

## 7. TEAM WORK

Nguzo ya saba ni **KUSHIRIKIANA NA WENGINE**, Hii kwa tafsiri ya shuleni ni kule

kusoma kwa kushirikiana na wengine kwa vikundi vya kujadiliana **{Group Discussion}.** Ili ufanikiwe kwenye masomo yako ni muhimu sana ujenge kawaida ya kujadiliana kuhusu masomo na wenzako, tafuta watu makini, wanaojali muda, wenye ndoto kubwa na wasio wababaishaji. Kwa kufanya hivyo **KUFAULU** ni lazima.

## 8. DISCIPLINE

Nguzo ya nane ni **NIDHAMU,** Hii ni kule kufanya jambo unalotakiwa kufanya hata kama hujisikii kufanya, yapo mambo mengi hayavutii kuyafanya ila usipoyafanya unafeli. Kwa mfano kuamka usiku kuacha usingizi na kwenda kusoma si jambo la kuvutia, ila ni lazima ufanye hivyo inapobidi ili ufanikiwe. Hivyo ni lazima uwe na nidhamu sana unapokua shuleni ili hii ikusaidie kufikia ndoto na malengo yako hata kama inaumiza.

## 9. EXECUTION

Nguzo ya tisa ni **KUMALIZA UNACHOFANYA**, Watu wengi huwa wanafeli sana kwa sababu huwa hawamalizi kile walichoanza kufanya, Ni muhimu sana kwako kujenga tabia ya kumaliza kila ulichoanza kufanya bila kuachia njiani kwa kukata tamaa au kurukia jambo lingine. Unaposoma hakikisha unajenga hii kawaida ya kumaliza jambo moja kabla

haujaanza jambo lingine. Hii itaongeza umakini na ufahamu kwa jambo ulilolianza na mwishowe ni **KUFANIKIWA**.

## 10. SHINNING

Nguzo ya kumi ni **KUNG'ARA,** Unaweza kuzingatia nguzo zote tisa na ukafikia hatua ya kung'ara, kwa maana ya kufaulu vizuri kwenye masomo yako, ila unaweza kujikuta unang'ara mara moja tu kisha ukazembea using'are tena. Hivyo ni lazima kung'ara kila wakati pia iwe ni nguzo yako. Hebu soma kwa sauti huu mstari wa Biblia hapa chini; -

***"Nami nilipofanikiwa nalisema sitaondoshwa milele" Zaburi 30:6.***

**Hizi ndiyo nguzo kubwa kumi za kuzingatia sana ili ufanikiwe kwenye masomo yako na maisha yako kwa ujumla.**

SURA YA 7

# MASWALI MUHIMU YA KUJIULIZA UNAPOELEKEA SEKONDARI.

Nimekuwa nikikupitisha kwenye maeneo mbalimbali ambayo tuna uhakika kwamba yamekusaidia sana kwenye safari yako ya mafanikio utakapokuwa sekondari. Sasa ni wakati wa sisi kukuuliza maswali ya kukusaidia kulingana na kile ulichokielewa.

Hebu chukua kalamu yako ya risasi[penseli] na anza kujaza nafasi zilizo wazi kwenye maswali nitakayokuuliza hapa chini.

**KUJENGA MSINGI;**

1. *Unadhani kuna umuhimu wowote kwa Wewe kujenga mahusiano mazuri na Mungu utakapokuwa shuleni? Kama NDIO unadhani ni KWANINI?*

…………………………………………………………

…………………………………………………………

…………………………………………………………

…………………………………………………………

…………………………………………………………

........................................................................
.........................

2. *Ni mambo gani unayotakiwa kufanya ili kuimarisha uhusiano wako na Mungu utakapokuwa shuleni na maisha yako yote?*

.......................................................
.......................................................
.......................................................
.......................................................
.......................................................
........................................................................
.......................

3. *Je, unadhani kuna jambo lolote ambalo linaweza kukuweka mbali na Mungu utakapokua shuleni? Kama lipo ni jambo gani?*

.......................................................
.......................................................
.......................................................
.......................................................
.......................................................
.......................................................
........................................................................
.............................

## ELIMU YA SEKONDARI NA MASOMO YAKE;

1. *Taja makundi makubwa matano ya Masomo yaliyopo sekondari.*

    i. ……..………………………………

    ii. ………………………………………

    iii. ………………………………………

    iv. ………………………………………

    v. ………………………………………

2. *Taja masomo manne yaliyopo kwenye kundi la Masomo ya Sayansi*

    i. ………………………………………

    ii. ………………………………………

    iii. ………………………………………

    iv. ………………………………………

3. *Taja masomo matano yaliyopo kwenye kundi la Masomo ya Sanaa*

    i. …………………………………............

    ii. …………………………………............

    iii. …………………………………............

    iv. …………………………………............

    v. …………………………………............

## DIRA, NDOTO na MALENGO YAKO;

1. *Ndoto na malengo yako ni kuwa.......................................*

2. *Je, ni masomo gani unatakiwa kuyazingatia ili kuitimiza ndoto yako?*

*Mchepuo wako ni.............................. wenye masomo..............................*

## MAMBO YA MSINGI SHULENI

1. *Taja mambo saba ya msingi ya kuzingatia utakapokuwa shuleni*
   - i. ..............................................
   - ii. ..............................................
   - iii. ..............................................
   - iv. ..............................................
   - v. ..............................................
   - vi. ..............................................
   - vii. ..............................................

1. *Taja mambo matano makubwa uliyojifunza juu ya haya mambo saba ya msingi ya kuzingatia utakapokua shuleni.*

   i. ............................................................
   ii. ............................................................
   iii. ............................................................
   iv. ............................................................
   v. ............................................................

## NGUZO KUBWA 10 ZA KUKUIMARISHA UNAPOKUWA SHULENI;

1. *Taja na eleza kidogo juu ya nguzo kubwa 10 za kukusaidia unapokuwa shuleni*

   i. ............................................................
   ............................................................
   ............................................................
   ............................................................
   ............................................................
   ii. ............................................................
   ............................................................
   ............................................................
   ............................................................
   ............................................................

iii. ............................................................
............................................................
............................................................
............................................................
............................................................

iv. ............................................................
............................................................
............................................................
............................................................
............................................................

v. ............................................................
............................................................
............................................................
............................................................
............................................................

vi. ............................................................
............................................................
............................................................
............................................................
............................................................

vii. ............................................................
............................................................
............................................................
............................................................

.......................................................

viii. .......................................................

.......................................................

.......................................................

.......................................................

.......................................................

ix. .......................................................

.......................................................

.......................................................

.......................................................

.......................................................

x. .......................................................

.......................................................

.......................................................

.......................................................

.......................................................